

Tanzia ya Mbebaji Ulinganizi

Mheshimiwa Al-Hajj Muhammed Naeem Muhammed Hasan (Abu Usamah Zukarnah) Mmoja wa Mashababu wa Hizb ut Tahrir

(Imetafsiriwa)

Kwa nyoyo zenye subira na matarajia mema, Hizb ut Tahrir / Wilayah ya Jordan inamuomboleza mbebaji da'wah, mmoja wa Mashababu wake wema, safi na mchamungu, na wala hatumtakasi yeyote mbele ya Mwenyezi Mungu, kutoka kizazi cha kwanza cha Hizb ut Tahrir, Al-Ustadh mwema:

Al-Hajj Muhammad Naeem Hasan (Abu Usamah Zakranah)

Ambaye aliregea kwenye rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu mnamo Jumapili asubuhi, 09 Muharram 1444 H sawia na tarehe 7 Agosti 2022 M, ambaye alitumia maisha yake kufanya kazi ya kusimamisha Khilafah kwa bidii na subira, kwa ahadi na kubeba ulinganizi, licha ya madhara na dhiki aliyokumbana nayo.

Mwenyezi Mungu amrehemu muheshimiwa ndugu Abu Usamah. Alikuwa mpole, mpenda dawah na Mashababu wake, mtenda kazi mwaminifu, mwenye msimamo juu ya haki, na akiifurahia ahadi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amsamehe na amrehemu na amkusanye pamoja na Manabii, wakweli, mashahidi na watu wema katika Pepo za neema, na hao ndio marafiki bora zaidi, na tunamuomba Mwenyezi Mungu aijaaliye familia yake subira, utulivu na faraja njema.

Ewe Mwenyezi Mungu, mrehemu ndugu yetu Abu Usamah, yakirimu makaazi yake, panua mlango wake, na umweke makaazi mazuri zaidi kuliko makaazi yake, na familia bora zaidi kuliko familia yake, na utokusanye sisi na yeye chini ya bendera ya Mtume wako Siku ya Kiyama.

**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir
katika Wilayah Jordan**